# UZINGATIAJI WA WATU WENYE ULEMAVU KATIKA SERA YA FEDHA NA MIPANGO

## ‘Taarifa Fupi’

Agosti 2021

WiLDAF TANZANIA
pact building local promise.
Freedom House

## Utangulizi

Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012 imeonesha kuwa idadi ya watu wenye ulemavu (WWU) ni 9.3% kati ya idadi watu nchini. WWU wanakumbana na changamoto mbalimbali za upatikanaji wa huduma za kifedha; ikiwamo utumiaji wa mashineza kieletroniki za utoaji fedha (ATM) na utumaji wa miamala kwa kutumia simu janja.

Sambamba na hilo, muundo wa sera za kifedha nchini Tanzania hautoi muongozo kwa watoa huduma za kifedha kuzingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu.

Taarifa hii fupi, inachambua juhudi za serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na taasisi zake katika kutekeleza sera ya fedha na mipango. Lengo kuu ni kuangalia ni kwa kiasi gani sera hizi zimejikita kuzingatia mahitaji ya WWU, kama ilivyoainishwa katika sheria na muundo wa Sera. Pia kutoa mapendekezo ya kuboresha sera ili ziweze kujumuisha watu wenye ulemavu katika masuala ya fedha.

## Maudhui

***Uzingatiaji wa mahitaji ya WWU (Mainstreaming of PWD)**, katika sekta za kifedha;ina maana ya kuboresha mifumo, upatikanaji wa taarifa, utumiaji wa mashine za kieletroniki za utoaji fedha* (ATM) pamoja na *kuboresha miundombinu mbalimbali ya kifedha kwa WWU.*

***Upatikanaji wa huduma za kifedha kwa WWU (Accessibility)**, ni uwepo wa urahisi wa mtu/watu kufikia huduma na bidhaa bila kuhatarisha af*ya, ustawi *na usalama wao.*

***Ujumuishaji (Inclusion)**, ni uwepo wa us*awa katika fursa za upatikanaji wa huduma za kifedha ili kuhakikisha kuwa kilamtu *anashiriki kikamilifu kwa kadri ya uwezo na matamanio yake.*

Sekta ya fedha nchini Tanzania imeweka mifumo mizuri ya sera, sheria, mipango na mikakati ya kitaifa inayozingatiwa. Hata hivyo, kwa upande wa WWU bado kuna mapungufu katika ujumuishaji wao katika sekta hii.

Mathalani, era ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2000 (**The National Micro-finance policy 2000)** imetoa huduma mbalimbali za kifedha ikiwamo; akiba, utoaji wa mikopo, malipo na huduma nyinginezo zinazo

wahusisha wafanyabiashara wadogo walioko mijini na vijijini. Sera hii imeweka mkazo katika usawa wa kijinsia na kuweka mapendekezo maalum yanayowezesha jamii kunufaika na huduma hizo. Hata hivyo, WWU hawajajumuishwa katika sera hii.

Hali kadhalika, Benki Kuu ya Tanzania (BOT) ni msimamizi mkuu wa huduma za kifedha nchini. BOT ina jukumu la kuhakikisha kuwa benki na taasisi za kifedha zinafanya kazi zake kwa kuzingatia Sheria ya WWU ya mwaka 2010. Hata hivyo, bado kuna changamoto kwa watoa huduma za kifedha katika utekelezaji ili kuhakikisha kuwa huduma hizo zinawafikia WWU.

Tanzania inatekeleza Mpango kazi wa ujumuishaji wa kifedha (NFIF 2018-2022), ambao umelenga kufanya huduma na bidhaa za kifedha ziweze kukidhi na kustawisha maslahi ya makundi maalumu (wanawake, vijana, wafanyabiashara na wakulima wadogo). Hata hivyo, mpango kazi huo haujajumuisha WWU.

## Mapungufu

Baadhi ya mapungufu yaliyopo katika kujumuisha mahitaji ya WWU katika sera ya fedha na mipango ya mwaka 2004 ni kama yafuatayo;

1. Miundombinu hafifu, mathalani mashine za kielektroniki (ATM), zenye urefu usio wezesha WWU kufikia na kupata huduma stahiki.
2. Ukosefu wa Sheria na Sera zinazosimamia masuala ya ujumuishaji wa WWU. Ingawa kumekuwa na ubunifu wa watu na mashirika binafsi ya kujali na kuzingatia mahitaji ya WWU.
3. Utoaji wa elimu na taarifa kwa wateja hauzingatii mahitaji maalum ya WWU.
4. Ukosefu wa kigezo cha masharti ya huduma jumuishi za WWU kama miongoni mwa sababu za kuzingatia kabla ya kibali cha huduma za kifedha kutolewa na Benki Kuu ya Tanzania (BOT).
5. Ukosefu wa usimamizi thabiti wa utekelezaji wa Sera na Sheria zinazohusu masuala ya ujumuishaji kikamilifu wa watu wenye ulemavu

## Juhudi za Serikali

Serikali imefanya juhudi kubwa katika kutengeneza Sera na Sheria ambazo zinawatambua na kuwalinda WWU. Juhudi hizo ni pamoja na Sera ya WWU ya Mwaka 2004 na Sheria ya WWU ya Mwaka 2010 ambazo kwa pamoja zimeainisha na kutambua ujumuishwaji na upatikanaji wa huduma za kijamii kwa WWU.

Kwa upande wa Sera, imesisitiza katika upatikanaji na ushiriki kikamilifu wa WWU katika jamii, pia imetoa rai kwa wadau kuhakikisha wanajenga miundombinu na kutoa huduma rafiki kwa watu wenye ulemavu. Vilevile, Sera hii imeainisha taarifa zinazotolewa kwa WWU kama moja ya njia kuu ya ushirikishwaji wao. Taarifa zinazotolewa na taasisi kwa Umma kama vile taasisi za kifedha zinapaswa kuwa ni za upatikanaji kwa WWU.

Tanzania ni nchi mwanachama wa mikataba ya kimataifa inayohimiza ujumuishaji wa WWU. Mikataba hii ni pamoja na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Watu wenye Ulemavu (UNCRPD) wa mwaka 2006 . Mkataba huu wa Haki za WWU umeainisha ujumuishwaji na ushirikishwaji wa WWU kama kanuni za msingi katika kutambua usawa na haki za binadamu. Hii inamaanisha, nchi mwanachama wa mkataba huu inapaswa kutambua na kuweka kwenye sheria zake za nchi hatua mahususi za kupinga na kuondoa kabisa aina zozote za unyanyasaji. Lengo ni kuweka mazingira rafiki kwa watu wenye ulemavu ili kuwawezesha kushiriki kikamilifu kwenye nyanja zote za kijamii.

Mkataba huu unatambua kuwa, chochote ambacho kinamzuia mtu mwenye ulemavu kufurahia uhuru na haki za binadamu ni ubaguzi. Hali kadhalika, mkataba huu unampa jukumu Waziri mwenye dhamana kuchukua hatua stahiki kupinga aina yoyote ya ubaguzi katika taasisi binafsi na za Umma. Hii ni pamoja na Waziri mwenye dhamana kuhakikisha miundombinu inayojengwa ni rafiki kwa watu wenye ulemavu kama ilivyoainishwa kwenye Ibara ya 40(1) ya mkataba huu.

Hata hivyo, mamlaka zenye dhamana pamoja na sekta ya fedha kiujumla hazijatekeleza matakwa ya Sera na Sheria ya WWU kwa kiwango cha kuridhisha, hasa katika kuzingatia ujumuishwaji wa WWU kikamilifu.

## Utendaji Mahiri Nchini Kenya

Sheria za fedha nchini Kenya (KBA namba 488) kama ilivyo Tanzania hazijaainisha bayana mahitaji muhimu ya watu wenye ulemavu kwenye huduma za kifedha. Hata hivyo, Jumuiya ya Mabenki nchini Kenya (KBA) inachukua hatua za makusudi kuhakikisha WWU wanajumuishwa kwenye mpango kazi wao. Huu ni mfano bora ambao nchi yetu ya Tanzania inaweza kutumia katika kuhakikisha haki za WWUzinazingatiwa.

Jumuiya ya Mabenki nchini Kenya (KBA) imejiwekea mkakati wa kutambua mahitaji ya WWU na kuwashirikisha katika kubuni njia bora za kuwajumuisha na kuwapa kipaumbele, ikiwa ni pamoja na kuwawezesha kutumia huduma za kifedha kwa uhuru bila vikwazo. Kwa mtazamo huo, wadau kwenye sekta ya fedha wamechukua hatua za makusudi katika kuhakikisha ushirikishwaji na uzingatiaji wa mahitaji ya WWU katika huduma za kifedha. Kwa hapa Tanzania, licha ya kuwa hakuna kifungu cha Sheria au Sera ya fedha kinachoruhusu unyanyasaji WWU, lakini bado WWU wanapitia vikwazo vinavyozuia uhuru wao katika kupata huduma za kifedha.

## Mapendekezo

Ili kukabiliana na mapungufu yaliyoainishwa hapo juu pamoja na kuwajengea WWU mazingira salama na rafiki katika kupata huduma za kifedha, Taarifa hii fupi inatoa wito kwa Wizara zenye dhamana pamoja na Taasisi za kifedha kama Benki kuu ya Tanzania kuchukua hatua zifuatazo;

1. Wizara ya fedha kufanya mapitio ya Sheria ya fedha ili kuweza kutambua watu wenye ulemavu katika upatikanaji na ufikiaji wa huduma hizo.

2. Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Vijana, Ajira, na Watu wenye Ulemavu kufanya mapitio ya sheria ndogo za fedha na benki ili kuweza kutambuaupatikanaji wa huduma kwa watu wenye ulemavu

3. Wizara ya Fedha kutoa maelekezo katika taasisi zote za fedha kama vile benki ili kuweza kuendana na Sera ya serikali katika utoaji wa huduma za kifedha hasa kwa watu wenye ulemavu.

4. Waziri wa Fedha kutoa muongozo kwa taasisi zote za kifedha kuhakikisha wanatoa mafunzo kwa wafanyakazi wao ili kuweza kutoa huduma rafiki kwa watu wenye ulemavu.

5. Benki Kuu ya Tanzania kutoa maelekezo kwa Taasisi zote zinazopewa leseni za kuendesha huduma ya kifedha kuhakikisha miundo mbinu na taarifa kwa wateja zinatolewa katika mfumo rafiki kwa WWU.

6. Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Vijana, Ajira na watu wenye Ulemavu izielekeze taasisi za kifedha kuhakikisha zinatekeleza takwa la sheria ya WWU 2010 inayotaka 3% ya waajiliwa kuwa ni WWU.

7. Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Vijana ,Ajira, na Watu wenye Ulemavu ifanye marekebisho ya Sera ya WWU kujumuisha upatikanaji wa huduma ya kifedha kwa WWU.

8. Wadau mbalimbali wa masuala ya WWU kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha kufanya utafiti kwenye taasisi za kifedha ili kubaini ni kwa kiwango gani huduma za kifedha zinapatikana kwa WWU.

9. Jumuiya za Mabenki waangalie uwezekano wa kuiga mfano wa Kenya katika kuwezesha upatikanaji wa huduma za kifedha kwa WWU.

## Kuhusu Shirika la Wanawake Katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika ( WiLDAF)

Shirika la Wanawake Katika na Sheria na Maendeleo Barani Afrika, ni mtandao wa mashirika yasiyo ya kiserikali unaotumia sheria kama nyenzo ya maendeleo kwa lengo la kuwajengea uwezo wanawake katika nyanja mbalimbali za kisiasa, kiuchumi, kijamii na kitamaduni.

Shirika lilianzishwa mnamo Februari 1990 huko Harare Zimbabwe - kufuatia mkutano wa Asasi za Kiraia uliofanyika katika muktadha wa muongo wa Umoja

wa Mataifa kwa wanawake ambapo ulibeba kauli mbiu “Haki za Wanawake na Maendeleo : Mtandao wa Uwezeshaji Barani Afrika”. Tangu wakati huo, Shirika limeanzisha matawi katika nchi 26 za Kiafrika, pamoja na Tanzania, ambazo zinajumuisha mashirika zaidi ya 350 na watu 3,000 ambao wanashiriki malengo haya.

## Kuhusu Mradi wa Uchechemuzi kwa Kutumia Takwimu (DDA)

Mradi wa uchechemuzi kwa kutumia Takwimu (DDA) ni mradi unaofadhiliwa na Shirika la Kimataifa liitwalo Freedom House pamoja na PACT Tanzania.

Mradi huu ambao ni wa miaka mitano unakusudia pamoja na mambo mengine kutumia takwimu kama sehemu ya kushawishi mabadiliko ya Sera na Sheria ambazo zinalinda na kutetea haki za binadamu.

Mradi huu unafanya kazi kwa kupitia vikosi kazi (WGs) mbalimbali. WiLDAF inaratibu kikosi kazi namba mbili (WG2) ambacho kimejikita katika kusimamia haki za Wanawake,Watoto, Vijana na watu wenye ulemavu.

## Shukrani

Taarifa hii fupi ni mchango wa watu binafsi, mashirika na wanachama wa kikosi kazi namba 2 ambao kwa pamoja wameshiriki katika kuandaa taarifa hii.

Kwa niaba ya kikosi kazi namba 2 (WG2), WiLDAF inapenda kutambua juhudi iliyofanywa na muandishi Bwana Novath Epimacus Rukwago kwa kujitolea kwake katika kuandaa taarifa hii fupi.

Shukrani za pekee ziende kwa Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Vijana ,Ajira, na Watu wenye Ulemavu kwa utayari wa kupokea taarifa na kutoa maoni ambayo yamesaidia kuboresha taarifa hii.

Mwisho, shukrani ziende kwa wanachama wa WG2 ambao wameshiriki kikamilifu katika kuandaa taarifa hii fupi kama ifuatavyo;

1. Women in Law and Development in Africa (WiLDAF),
2. Tanzania Child Right Forum (TCRF),
3. Tanzania Domestic Workers Coalition (TDWC),
4. Mwanza Children and Youth Network (MCYN),
5. Tanzania Early Childhood Development Network (TECDEN),
6. Zanzibar Female Lawyers Association (ZAFELA),
7. Tanzania Association for children Advancement (ZACA),
8. Women Legal Aid Centre (WLAC),
9. Women with Disability Network (SHIVYAWATA),
10. Youth Partnership countrywide (YPC),
11. Gender and Adolescence Initiative (GAI)
12. Vijana Pambana Pata Maendeleo Rukwa (VIPAMARU),
13. Jitambue Lembuka,
14. Health Integrated Multispectral Services (HIMS),
15. Women Development for Science and Technology Association (WODSTA).

**Imechapishwa na WiLDAF, 2021**
Women in Law and Development in Africa.
Eneo la Mikocheni A. Mtaa wa WiLDAF, Block F. Ploti Na. 635.
S.L.P 76215, Dar es salaam, Tanzania

**Simu:** +255222701995,
**Barua pepe:** wildaftanzania@gmail.com / info@wildaftanzania.or.tz
**Tovuti:** www.wildaftanzania.or